SWALI: Nini maana ya huu mstari?

> *Mithali 14:23 “Katika kila kazi mna faida; Bali maneno ya midomo huleta hasara tu”*
>
> _____

JIBU: Kitabu cha Mithali na Mhubiri ni vitabu vilivyobeba mafunzo mengi sio tu yale ya kiroho bali pia hata ya maisha ya kawaida. Mstari huo unaelezea uzito wa kitu kinachotendewa kazi zaidi ya kile kinachozungumzwa tu. Kwamfano hapo anaanza kwa kusema “katika KILA KAZI mna faida”.. Maana yake ni kuwa katika kazi yoyote (iliyonjema), inafaida nyuma yake,. Iwe ni ya kudharaulika au yenye heshima, iwe ni ngumu iwe ni rahisi, iwe ni ya kipato kikubwa au kidogo, maadamu kazi fulani inatendeka ni lazima faida tu itaonekana nyuma yake.

Lakini mtu akiwa ni wa mipango mikubwa, mikakati mingi, akili nyingi za kubuni namna ya kutenda kitu Fulani, vikao vingi, halafu hakitendei kazi, Bwana anasema, badala ya faida kinyume chake ni hasara tu atapata..

Vivyo hivyo na katika roho. Bwana anataka tuwe watendaji wa Neno lake, Sio kusikia tu au kuomba tu peke yake. Unaweza ukaomba usiku kucha lakini kama sio mtendaji wa Neno lake uliombalo, ni unapoteza nguvu tu.

Kwamfano unaomba Bwana akusaidie uushinde uasherati, lakini bado unashikamana na vichocheo vyake vyote, una picha chafu kwenye simu yako, kinywa chako kinazungumza mambo ya kizinzi na vijana wenzako, unachati na watu wa jinsia tofauti muda wote, unatazama tamthilia zenye maudhui hayo, unasikiliza miziki ya kidunia, unaishi na boyfriend/girlfriend. Unategemea vipi tamaa zisikutawale? Utaomba usiku kucha na hutaona matokeo yoyote, kwasababu hukitendei kazi kile unachokiomba.

Bwana alisema kama vile mwili bila roho umekufa, vivyo hivyo imani bila matendo imekufa ndani yake.(Yakobo 2:17). Kukitendea kazi kile kimoja ukiombacho, kina nguvu sana kuliko maneno elfu unayoweza kumwomba Mungu mwaka mzima.

> *Yakobo 1:22 “Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu. 23 Kwa sababu mtu akiwa ni msikiaji wa neno tu, wala si mtendaji, mtu huyo*

> *ni kama mtu anayejiangalia uso wake katika kioo. 24 Maana hujiangalia, kisha huenda zake, mara akasahau jinsi alivyo”.*

Shalom.

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:
Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au
Piga namba hizi: +255693036618 au +255789001312

Mada Nyinginezo:

Nini maana ya “katika wingi wa hekima mna wingi wa huzuni”.[1]

Nini maana ya huu mstari? “Yeye mwenyewe ataokolewa lakini ni kama kwa moto”[2]

Mithali 14:4 ‘Zizi ni safi ambapo hapana ngombe;[3]

Marijani ni nini katika biblia(Ayubu 28:18,Mithali 8:11)?[4]

Nini maana ya mhubiri 9:11? si wenye mbio washindao katika michezo?[5]

BWANA UNIJULISHE MWISHO WANGU.[6]

Rudi nyumbani[7]

Share on:
WhatsApp
Endnotes:

1. Nini maana ya “katika wingi wa hekima mna wingi wa huzuni”.: https://wingulamashahidi.org/2020/10/10/nini-maana-ya-katika-wingi-wa-hekima-mna-wingi-wa-huzuni/
2. Nini maana ya huu mstari? “Yeye mwenyewe ataokolewa lakini ni kama kwa moto”: https://wingulamashahidi.org/2022/03/07/nini-maana-ya-huu-mstari-yeye-mwenyewe-ataokolewa-lakini-ni-kama-kwa-moto/
3. Mithali 14:4 ‘Zizi ni safi ambapo hapana ngombe;: https://wingulamashahidi.org/2019/09/01/zizi-ni-safi-ambapo-hapana-ngombe/
4. Marijani ni nini katika biblia(Ayubu 28:18,Mithali 8:11)?: https://wingulamashahidi.org/2020/09/25/marijani-ni-nini-katika-bibliaayubu-2818mithali-811/
5. Nini maana ya mhubiri 9:11? si wenye mbio washindao katika michezo?: https://wingulamashahidi.org/2021/03/12/nini-maana-ya-mhubiri-911-si-wenye-mbio-washindao-katika-michezo/
6. BWANA UNIJULISHE MWISHO WANGU.: https://wingulamashahidi.org/2022/12/01/bwana-unijulishe-mwisho-wangu/
7. Rudi nyumbani: https://wingulamashahidi.org